

# Nishani ya Nyasi.


Nishani hii ipo katika kundi la viumbe vya asili, huwakilishwa kwa rangi nyeupe

By: Yusuph Mwasiposya

## Utangulizi

- Nyasi ni nini?

Nyasi ni mmea ulio na mbegu zenye ghala moja (monokotiledoni)




2


## Sifa za nyasi

- Nyasi nyingi ni za misimu
- Vena za majani yake vimenyooka
- Nyasi zina mizizi yenye nyuzinyuzi
- Nyasi zina mizizi iliyotawanyika
- Nyasi hazina mzizi mkuu
- Nyasi zina mbegu zenye ghala moja (monokotiledoni)
- Majani huchukua sehemu kubwa sana ya mmea

3

## Sifa za nyasi

- Nyasi nyingi huwa na shina fupi lililofunikwa na majani
- Nyasi zina photosynthesis bora zaidi




4

## Mizizi ya nyasi

- Mizizi ya nyasi huitwa rhizome.
- Mizizi hii hutambaa kwa ulalo na kisha huweza kutoa vichipukizi kutoka katika mizizi yenyewe
- Mara nyingi mizizi hii hutumika kama mbegu kwa ajili ya kuzalisha nyasi nyingi zaidi.


5

## Aina za nyasi

- Kuna aina zaidi ya 10,000 za mimea jamii ya nyasi
- Nyasi huchukua karibu 20% ya ukijani wote katika uso wa dunia
- Nyasi ndio mmea ulio na mchango mkubwa kwa shughuli za kiuchumi kwa binadamu kuliko mmea wowote

6

*Grasslands (ardhi ya nyasi)*




Sababu za kudumu kwa nyasi

Pamoja na kukatwa mara kwa mara, kuchomwa mote, au kuliwa na Wanyama, nyasi huweza kuota tena kwa haraka bila kunyauka kwa sababu majani yake hukua toka chini na si kutoka katika kikonyo pekee.



8

Nyasi za msimu

- Ni nyasi zinazoota, kukua, kutoa mbegu na kisha kunyauka ndani ya kipindi imoja katika mwaka.
- Mfano wa nyasi hizo ni: mahindi, ngano, mtama, uwele, mchele, shayiri n.k

9

Nyasi za mwaka mzima

- Hizi ni nysi ambazo huwa hai nyakati zote za mwaka, ingawa majani yake yanaweza kunyauka lakini mizizi yake hupaki kuwa hai mwaka mzima
- Mfano wa nyasi hizi ni: Sudani, mianzi, ukoka, mafunjo n.k

10

Bidhaa zitokanazo na nyasi

- Mkate: ngano, shayiri, mahindi
- Fagio: mafunjo
- Fimbo za ndoano: mianzi
- Gluteni: ngano, shayiri
- Vileo: ngano, shayiri, mahindi, mtama
- Nyasi za kuezekea: shayiri, timothy
- Uji: mahindi
- Ugali: mahindi, ngano, mtama, uwele

11

Bidhaa zitokanazo na nyasi

- Molasi: miwa, mtama
- Sukari: miwa, mahindi
- Stachi: mahindi, ngano, mpunga
- Unga wa shayiri: shayiri
- Unga mweupe kwa ajili ya kuoka: ngano, mahindi

12

## Mahitaji muhimu

- Kusanya aina kumi za nyasi zilizopo katika maeneo yako kisha uziwekee maelezo mafupi kuonesha jina la nyasi, siku uliyokusanya na uoneshe angalau kazi moja ya nyasi hiyo

13

## Mahitaji muhimu

- Andika insha ya ukurasa mmoja kuhusu matumizi ya nyasi katika shughuli mbalimbali duniani

Insha yako ijumuishe vitu vifuatavyo:

- Matumizi makubwa ya nyasi kwa binadamu
- Chakula kikuu cha Tanzania
- Faida za nyasi
- Hasara za nyasi

14

## Faida za nyasi

- Hutupatia kipato
- Huzuia mmomonyoko wa udongo
- Hutunza rutuba ya ardhi
- Hutupatia chakula
- Hulisha mifugo
- Hutumika kuezekea majengo
- hutupatia vituo vya mapumziko
- Hupunguza hewa ya ukaa angani
- Husaidia udongo kutunza maji

15

## Hasara za nyasi

- Huficha wadudu na wanyama waharibifu mf: nyoka
- Huota kama magugu shambani
- Kuna baadhi ya nyasi huweza kumkata mtu na kumuumiza
- Zikiota hovyo huchafua mazingira

16

## Nyasi katika biblia

- Mwanzo 41:2 – nyasi ni chakula cha Wanyama
- Kutoka 2:3 – Musa alifichwa katika kisafina cha manyasi
- Ayubu 41:27 – Mungu huona chuma kama nyasi
- Isaya 19:6 – Miongoni mwa laana anazotoa Mungu ni kukausha nyasi zinazotoa chakula kikuu kwa watu
- Isaya 35:7 – miongoni mwa baraka ambazo Mungu anaahidi ni kufanya nyasi kumea mahali zisipoweza kumea

17

## Rejea

Retrieved from "https://en.wikibooks.org/w/index.php?title=Adventist_Youth_Honors_Answer_Book/Nature/Grasses&oldid=3250898"

18